# Mabadiliko ya hali ya hewa yazidi kuwa tishio duniani

NA ANGELA SEBASTIAN, BUKOBA

**DUNIA inalia. Kila nchi inalia. Watu wanalia. Wanyama, mimea na viumbe hai vinalia. Vinalilia maisha. Mazingira wanayoishi yako hatarini.**

Juhudi zisipochukuliwa kupambana na uharibufu wa mazingira ili kuepuka mabadiliko ya hali ya hewa nchi itaingia katika janga ambalo kila mtu atalia na kusaga meno.

Ni kweli kila mmoja achukue hatua, kwani kutachangia kuepusha kuangamia. Juhudi za kujengeana uwezo juu ya mabadiliko ziwe wazi kwa kila mtu.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanachukua muda mrefu kuonekana na matokeo yake ni kuongezeka kwa joto, mvua zisizo na msimu, upepo, na kukosekana kwa msimu sahihi wa kilimo.

Ofisa kutoka shirika lisilo serikali la Vi Agroforesty linalojishughulisha na uhifadhi wa mazingira na misitu nchini, Abubakar Munga, wakati akitoa elimu juu ya mabadilko ya hali ya hewa kwa wananchi wa wilaya ya Karagwe alisema kila mwananchi anatakiwa kutunza mazingira.

Munga anasema Intergovermental Panel on Climate Change (IPCC) ni chombo cha kimataifa kinachoshughulikia utoaji taarifa ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Anasema utafiti wa IPCC unaonyesha kuwa kwa kipindi cha karne moja yaani tangu 1906 hadi 2005 wastani wa joto duniani umeongezeka toka nyuzi joto 0.5 hadi 0.7.

Tafiti zinaonyesha kuwa wananchi wangetegemea kuwepo na ongezeko la nyuzi joto 1.1 hadi 6.4 ifikapo 2010. Hiyo ni kwa mujibu wa utafiti wa IPCC wa mwaka 2007.

Anasema shughuli za maendeleo ya binadamu kama vile uchomaji wa mafuta ghafi na ukataji wa misitu zinazidisha tabaka katika angahewa ambalo hutokana na kuongezeka kwa gesi joto na hivyo kuongeza joto katika sura ya dunia zaidi ya kiwango cha kawaida.

Anaeleza kwamba shughuli za binadamu kama mapinduzi ya viwanda, uharibifu wa misitu na kilimo huchangia kuongezeka kwa joto zaidi katika sura ya dunia.

MAMBO YA KUZINGATIA

Anatoa ushauri kuwa mambo ya kuzingatia katika kuzuia uharibifu wa mazingira ni kuzuia uharibifu wa ardhi, na kuzuia ongezeko la gesi joto kwa kutokata mito hovyo.

Njia nyingine za kuzingatia ni kupunguza biashara ya magogo, ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa, uchomaji moto holela, na shughuli za migodi ya madini, na kupunguza mifugo.

Madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira ni pamoja na upotevu wa rutuba, kupungua kwa maeneo yanayofaa kwa kilimo, kujaa kwa taka katika mito, maziwa na bahari.

Pia upungufu wa kuni, mbao na mazao ya misitu, ongezeko la mafuriko, kukauka vyazo vya maji, kuongezeka kwa magonjwa na ukame.

Anaeleza mabadiliko ya hali ya hewa yataathiri afya za wananchi kutokana na ongezeko la magonjwa kama kipindupindu na malaria, hivyo kufanya maisha kuwa magumu.

Kukosekana kwa mvua za kutosha na ongezeko la ukame huchangia lishe duni hivyo huongeza kiwango cha vifo vya watoto.

Anaeleza mabadiliko ya hali ya hewa yatakuwa na athari kubwa katika upatikanaji wa maji nchini kutokana na ukame.

Munga anasema Ziwa Victoria linalotumiwa na Kenya,Tanzania na Uganda linakabiliwa na matatizo mengi kama vile uchafuzi mazingira kutokana na majitaka na uvuvi haramu, vitu ambavyo vinaleta tishio kwa ziwa hilo.

Anasema tafiti zinaonyesha kwamba kwa sasa asilimia 30 ya samaki wa maji baridi na zaidi ya spishi nyingine 800 za maji baridi ziko katika hatari ya kutoweka kwenye maziwa ya Africa.

"Hivi karibuni shughuli za uvuvi zimekuwa ngumu sana kwa kuwa kuna uvuvi haramu. Watu wengi wanavua samaki katika eneo moja.

"Mwaka 1992 kina cha ziwa kilikuwa cha kawaida kisha kilipungua kuelekea mwishoni mwa miaka ya 1990 na Elnino ilipotokea mwaka 1998, ziwa lilifurika kuzunguka maeneo,lakini tangu 2000 ziwa limepungua sana,"anasema Munga.

Munga anasema serikali wilaya ya Karagwe imewaagiza wananchi kuhakikisha wanatunza mazingira ikiwa ni pamoja na kupanda miti ili kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ofisa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dk Robart Ntakamulenga anasema sera ya taifa ya mazingira ya mwaka 1997 imebainisha matatizo makubwa ya kimazingira nchini na yanayohitaji ufumbuzi wa haraka.

Matatizo hayo ni pamoja na uharibifu wa ardhi, ukosefu wa maji safi na salama mijini na vijijini, uchafuzi wa mazingira , uharibifu wa mifumo ya majini na ukataji wa misitu.

Anasema umuhimu wa mazingira kwa uchumi wa Tanzania uko katika sura nne: Mazingira yanaipatia nchi mahitaji ya msingi kwa ajili ya kufanikisha masuala ya jamii na uchumi.

Mazingira ndio makazi ya viumbe vyote. Mimea na wanyama ambao ndio urithi usiokuwa na mbadala, mazingira ni chombo cha kuweka yale yasiyofaa na ni msingi wa kupunguza unyonge wa umasikini.

Ni dhahiri kwamba msukumo mkubwa wa uongozi wa mazingira ni kulinda sehemu asili ya kuishi binadamu na kuoanisha upungufu uliopo kwenye mazingira katika kusaidia kufikia uamuzi sahihi.

Katika kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya 1997, Sheria Namba 20 ya mwaka 2005 ya Usimamizi wa Mazingira ilitungwa na kupitishwa na Bunge, ambapo ilianza kufanya kazi Julai Mosi, 2005.

Anaeleza kuwa madhumuni ya sheria hiyo ni kuweka muundo wa kisheria na kiasasi katika usimamizi endelevu wa mazingira ambapo kanuni kadhaa zimekwishaandaliwa na nyingine ziko katika maandalizi;

Dk Ntakamulenga anasema wananchi wanahakikishiwa haki yao ya kushiriki na kutoa uamuzi katika utengenezaji wa sera ya mazingira, malengo, mipango na kuwashirikisha katika utayarishaji wa sheria na kanuni zinazohusu mazingira.

Pia inahusu kuanzishwa kwa mazungumzo na nchi jirani juu ya uanzishaji wa programu za usimamizi wa mazingira kwa ajili ya kuondoa na kupunguza uharibifu unaoweza kutokea katika maeneo yanayovuka mipaka lakini yanayoshabihiana kimazingira.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanazidi kuonyesha madhara yake ambapo mvua zinazidi kunyesha katika jiji la Dar es Salaam. Mvua hizo zimesababisha madhara kwa watu kupoteza makazi na maisha.

Pamoja na Mamlaka ya Hali ya Hewa chini kutoa taarifa za kuwepo kwa mvua kubwa msimu huu, lakini utabiri huo mara nyingi haundeni na kile kinachotokea baadaye.

Hiyo inachangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa na hivyo kujikuta mvua ikinyesha kwa wingi tofauti na matarajio yaliyozoeleka. Kwa kuwa huwa hakuna maandalizi ya kukabiliana na mvua za namna hiyo, matokeo yake ni madhara makubwa kwa watu na taifa■



*UKATAJI miti hovyo huchangia uhalibifu wa mazingira. Juhudi zinahitajika kuyatunza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.*